

MAIR

Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji
MKUKUTA - 2006/2007



Ijue MAIR

Ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa MKUKUTA (MAIR—MKUKUTA Annual Implementation Report) ni moja ya matokeo ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA. Ripoti hii ni sehemu ya muundo wa jumla unaohusisha taarifa za wadau wanaohusika na utekelezaji wa MKUKUTA ambao ni pamoja na Wizara, Idara, na wakala wa serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Asasi Zisizo za Serikali (AZISE).

Masuala Makuu ya MAIR ni:

- MAIR ni uchambuzi wa maendeleo kwa kuzingatia malengo ya MKUKUTA na kutoa picha halisi ya utekelezaji, changamoto, mambo ya kujifunza na hatua za kuchukua katika siku zijazo kwa kila nguzo ya MKUKUTA
- Inajumuisha taarifa za maendeleo ya michakato na maboresho ya Wizara, Serikali za Mitaa na AZISE na kubainisha mchango wa kila moja katika kufikia matokeo ya MKUKUTA.
- Mchango wa AZISE mara nyingi hauwekwi bayana, hata hivyo izingatiwe kwamba serikali inatambua mchango mkubwa wa sekta hii.
- Ripoti za maeneo mengi hutegemea taarifa na takwimu za shabaha za utekelezaji. Taarifa hizi huwa ama tarakimu au maelezo kutegemeana na upatikanaji wa takwimu.
- Mafanikio yaliyopatikana katika masuala mtambuka yamejumuishwa kwenye uchambuzi wote wa mafanikio yaliyopatikana.

MAIR ina Madhumuni Makuu Mawili:

- Kuwafahamisha wadau na Watanzania wote kwa ujumla kuhusu mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa MKUKUTA pamoja na michakato inayohusika. Hili linaweza kufanyika moja kwa moja ama kupitia wawakilishi wa wadau au wananchi kama vile Wabunge.
- Kuchochea mijadala katika masuala ya msingi, na hivyo kusaidia kushawishi na kuboresha mipango, bajeti na utekelezaji wake.

Malengo Makuu na Matumizi ya Ripoti hii:

- Kupima mafanikio dhidi ya vipaumbele vya Serikali kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umaskini kama vilivyoainishwa ndani ya MKUKUTA.
- Kuwezesha kupatikana kwa taarifa zitakazosaidia kubuni mbinu na kuweka vipaumbele katika sekta mbali mbali ili ziweze kuwa thabiti na endelevu.
- Kuchochea mijadala na midahalo zaidi miongoni mwa wadau kuhusu masuala ya kimkakati. Hii inaweza kuhusisha; (a) kuweka na kupanga vipaumbele na utafutaji raslimali na (b) namna bora ya kutumia mijadala ya siku za baadaye.
- Kubainisha masuala muhimu pamoja na njia tofauti za kuongeza raslimali ili kufikia malengo na shabaha za MKUKUTA.
- Kuzalisha taarifa ili kusaidia kuboresha mchakato wa kitaifa wa uandaaji bajeti.

Mipaka na Mapungufu ya MAIR:

Tangu mwanzo, MAIR imekuwa na kiu kubwa. Ilikusudia kutoa taarifa kwa mpangilio na za kina kuhusu matumizi, shughuli, na matokeo pamoja na matunda ya matokeo hayo. Hii ingehusisha taarifa za kina kuhusu mambo ambayo serikali ilipanga kufanya, kiasi cha raslimali kilichopangwa na kutumika, shughuli zilizotekelezwa na hatua zipi zilichukuliwa. Lakini kutokana na sababu zifuatazo, MAIR 2006/07 haikidhi matarajio yote haya:

- Licha ya bajeti za Wizara, Idara na Wakala na Serikali za Mitaa kufungamanishwa na MKUKUTA kwa kiasi kikubwa, njia ya sasa ya utoaji ripoti juu ya namna bajeti inavyotumika haijafungamanishwa kikamilifu na malengo ya kimkakati na matokeo ya MKUKUTA.
- Ukosefu wa takwimu kwa baadhi ya viashiria ambavyo takwimu zake hazikusanywi mara kwa mara.

- Kwa baadhi ya maeneo kama vile utamaduni, mfumo wa ufuatiliaji bado haujaweka viashiria vya matokeo. Hata hivyo, kila inapowezekana, shughuli na michakato inayohusika kwenye maeneo hayo imeripotiwa.

Kwa ufupi, MKUKUTA:

- Ni Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini kwa kipindi cha kuanzia 2005/2006 hadi 2009/2010
- Ni uzao wa pili wa Waraka wa Upunguzaji Umaskini. Uliandaliwa kufuatia mapitio ya Mkakati wa kwanza wa Upunguzaji wa Umaskini wa mwaka 2000 yaliyohusisha mashauriano ya wadau wengi.
- Umekusudiwa kuwa muundo wenye kuoanisha mipango, bajeti, utekelezaji, ufuatiliaji na taarifa za wadau wengi.
- Hupitiwa na Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA (MMS) ambao huongozwa na Mpango Mkuu wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA (MMMP)
- Huongozwa na Kamati ya Ufundi. Husimamiwa na Sekretarieti. Huendeshwa na makundi matatu ya Kiufundi 'Utafiti na Uchambuzi', 'Tafiti na Takwimu za kila siku za kiutawala' na 'Mawasiliano'
- Unagharamiwa na Serikali kwa msaada wa Wabia wa Maendeleo pamoja na Wadau wengine.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Wizara ya Fedha na Uchumi,
S..L.P. 9111, Dar Es Salaam

Simu: +255 2111174, Fax: 21103226

Barua Pepe: mkukuta@gmail.com; Tovuti: www.povertymonitoring.go.tz